# Barua ya Kuwakaribisha Wazazi
# Idara ya Huduma za Chakula na Lishe

Althea Albert-Santiago, Mkurugenzi wa Huduma za Chakula na Lishe **(314) 345-4519 x74519**
Tenecia Williams, Mtaalamu wa Uwajibikaji **(314) 345-2308 x72308**
Erika Hollinshed, Mtaalamu wa Upishi **(314) 331-6115 x 76115**

---

Saint Louis Public Schools (SLPS) na Southwest Foodservice Excellence (SFE),LLC zinaamini kwamba mojawapo ya njia muhimu zaidi tunayoweza kuwasaidia wanafunzi kufanya vyema katika madarasa yao ni kuwapa chakula chenye afya na kizuri. ***Tafadhali kumbuka kuwa bei zinaweza kubadilika.***

**<u>Mpango wa Kutoa Chakula Kwa Jumuiya Zinazostahiki:</u>**

Saint Louis Public Schools iko chini ya Mpango wa Kutoa Chakula Kwa Jumuiya Zinazostahiki ambao unawaruhusu wanafunzi wote wa shule ya SLPS kupata kiamsha kinywa, chakula cha mchana, chakula cha jioni na vitafunio bila kukamilisha Ombi la Familia la Kupewa Chakula.

**Idara ya Huduma za Chakula na Lishe inasimamia Mipango ifuatayo ya Lishe ya Mtoto inayofadhiliwa na Idara ya Kilimo ya Marekani (USDA), Idara ya Elimu ya Msingi na Sekondari (DESE), na Idara na Afya na Huduma kwa Wazee ya Missouri**

- Mpango wa Kuwapa Wanafunzi Kiamsha kinywa Shuleni (SBP)
- Mpango wa Kitaifa wa Kuwapa Wanafunzi Chakula cha Mchana Shuleni (NSLP)
- Mpango wa Kuwapa Wanafunzi Matunda na Mboga (FFVP)
- Mpango wa Kuwapa Wanafunzi Vitafunio Baada ya shule (ASP)
- Vitafunio Vinavyouzwa ili Kuchangisha Pesa/Michango
- Mpango wa Utunzaji wa Kuwapa Chakula Watoto na Watu Wazima (CACFP)
- Mpango wa Kuwapa Wanafunzi Chakula Katika Majira ya Joto

**<u>Mpango wa Kuwapa Wanafunzi Kiamsha kinywa Shuleni:</u>**

- Kiamsha kinywa kinatolewa kwa wanafunzi wote bila malipo. **Watu Wazima Hulipia: <u>$2.50</u>**
- Kiamsha kinywa hutolewa kabla ya kuanza kwa vipindi vya masomo katika madarasa na kafeteria
- Chaguo la kinywaji moto au nafaka kila siku, matunda au juisi ya 100%, maziwa yenye mafuta kidogo ya 1% au maziwa yasiyo ya mafuta
- **Maziwa yoyote ya ziada yanaweza kununuliwa: maziwa pekee- $.55 yaliyo na chokoleti: -$.60**
- Menyu ziko kwenye tovuti ya Saint Louis Public Schools(www.slps.org/menus)

**<u>Mpango wa Kitaifa wa Kuwapa Wanafunzi Chakula cha Mchana Shuleni:</u>**

***<u>Shule za Msingi:</u>***

- Chakula cha mchana kinatolewa kwa wanafunzi wote bila malipo. **Watu Wazima Hulipia: <u>$4.15</u>**
- Chakula cha mchana ni pamoja na chaguo la vyakula moto vyenye afya, bidhaa za nafaka, matunda, mboga, vyakula vya mboga mboga, na ya maziwa yenye mafuta kidogo ya 1% au maziwa ya chokoleti yasiyo na mafuta
- Milo hutolewa katika madarasa na kafeteria
- **Maziwa yoyote ya ziada yanaweza kununuliwa: maziwa pekee- $.55 yaliyo na chokoleti: -$.60**
- Menyu zinapatikana kwenye tovuti ya Saint Louis Public Schools(www.slps.org/menus)

***<u>Shule za Kati:</u>***

- Chakula cha mchana kinatolewa kwa wanafunzi wote bila malipo. **Watu Wazima Hulipia: <u>$4.15</u>**

- Chakula cha mchana ni pamoja na chaguo la vyakula moto vyenye afya, bidhaa za nafaka, matunda, mboga, vyakula vya mboga mboga, na ya maziwa yenye mafuta kidogo ya 1% au maziwa ya chokoleti yasiyo na mafuta
- **Maziwa yoyote ya ziada yanaweza kununuliwa: maziwa pekee- $.55 yaliyo na chokoleti: -$.60**
- Menyu zinapatikana kwenye tovuti ya Saint Louis Public Schools (www.slps.org/menus)
- Kila mwanafunzi atatumia vitufe kuweka Nambari yake ya Utambulisho wa Kibinafsi (PIN) anapopokea kiamsha kinywa na chakula cha mchana. PIN itasalia kuwa ile ile kila mwaka.

***Shule za Upili:***

- Chakula cha mchana kinatolewa kwa wanafunzi wote bila malipo. **Watu Wazima Hulipia: $4.15**
- Chakula cha mchana ni pamoja na chaguo la vyakula moto vyenye afya, bidhaa za nafaka, matunda, mboga, vyakula vya mboga mboga, na maziwa yenye mafuta kidogo ya 1% au maziwa yasiyo na mafuta
- Matunda na aina tofauti za mboga kwa chaguo za chakula chenye afya
- **Maziwa yoyote ya ziada yanaweza kununuliwa: maziwa pekee- $.55 yaliyo na chokoleti: -$.60**
- Menyu zinapatikana kwenye tovuti ya Saint Louis Public Schools (www.slps.org/menus)
- Kila mwanafunzi atatumia vitufe kuweka Nambari yake ya Utambulisho wa Kibinafsi (PIN) anapopokea kiamsha kinywa na chakula cha mchana. PIN itasalia kuwa ile ile kila mwaka.

**Mpango wa Utunzaji wa Kuwapa Chakula Watoto na Watu Wazima (CACFP): Mpango wa Kuwapa Wanafunzi Chakula cha jioni Baada ya shule**

- Mpango wa Kuwapa Wanafunzi Chakula cha Jioni Baada ya Shule unaofadhiliwa na Idara ya Afya na Huduma kwa Wazee ya Missouri
- Wanafunzi hupewa chakula cha jioni chenye lishe bora na vitafunio
- Shule zinazotoa mipango ya baada ya shule inayojumuisha mipango ya elimu, masomo ya ziada na michezo zinastahiki kushiriki
- Shule zinaweza kupokea chakula baridi au moto

**Maelezo ya ziada ya lishe:**

- Tembelea tovuti ya SLPS: www.slps.org
- Ili kusoma muhtasari wa huduma za Idara ya Huduma za Chakula na Lishe, tembelea: www.slps.org bofya **Kichupo cha Mzazi (Parent) na Mwanafunzi (Student)**, kisha uende kwenye **Muhtasari (Overview).**
- Ili kusoma **Sera ya Chakula na Menyu na Barua ya Kukaribisha Wazazi** katika lugha zingine, **tembelea,** www.slps.org, bofya **Kichupo cha Mzazi (Parent) na Mwanafunzi (Student)**, kisha uende kwenye **Sera ya Chakula na Menyu.**
- Ili kusoma Sera ya Afya na Siha, au kusoma Sera katika lugha zingine, tembelea: www.slps.org, bofya Kichupo cha **Parent & Student**, kisha uende kwenye **Health and Wellness.**
- Ili kukagua maelezo kuhusu Nambari za Utambulisho wa Kibinafsi (PIN), **tembelea** www.slps.org, bofya Kichupo cha **Parent & Student**, kisha uende kwenye **Meal Policy and Menus**

Tafadhali wasiliana na Idara ya Huduma za Chakula na Lishe kwa (314) 345-4519 au (314) 345-2308 ikiwa una maswali yoyote.

Wenu Mwaminifu,

*Althea Albert-Santiago, MPH, CCNP, CMP* Mkurugenzi wa Huduma za Chakula na Lishe

**Shule hii inatoa fursa sawa kwa wote.**